**5 JUNI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 5 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 530

### Kuongeza Watu Wasio na Ulemavu katika Vyuo vya Watu Wenye Ulemavu

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza watu wasio na ulemavu kujiunga na vyuo vya watu wenye ulemavu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM K.n.y. WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa miaka mitano 2021/2022 – 2025/2026. Pia Serikali imeandaa Mwongozo wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi 2022/2028 wa Oktoba, 2022. Aidha, Serikali inatekeleza Mpango Mkakati wa Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu 2023/2024 – 2025/2026 ambapo pamoja na mambo mengine unahusu suala la elimu na ujuzi kwa kuzingatia ujumuishaji wa watu wenye na wasio na ulemavu katika maeneo ya kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwaandaa wanafunzi kuishi maisha jumuishi katika jamii imeandaa mikakati na miongozo kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wenye ulemavu wanajifunza na kuishi katika mazingira yanayowaunganisha na jamii nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mpango Mkakati wa Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu wa mwaka 2023/2024 – 2025/2026, Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kudahili wanafunzi 2,000 kupitia vyuo vya watu wenye ulemavu, kati yao wasio na ulemavu ni 400 hii ni 20% ya wanafunzi wote. Aidha, mwaka 2024/2025 Serikali imepanga kupitia vyuo vyake vya watu wenye ulemavu kudahili wanafunzi 1,500 kati yao wasio na ulemavu ni 500 sawa na 30% ya wanafunzi wote, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa ruhusa yako naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuboresha vyuo vyote vya wenye

ulemavu ikiwemo kile cha Yombo, Ilala - Dar es salaam, Masiwani – Tanga na Luwanzari - Mwanza vyuo hivi vilikuwa katika hali mbaya na sasa vina mazingira mazuri sana pongezi kwake Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kulijali kundi hili muhimu la watu wenye ulemavu. Sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kwenye vyuo hivi vya wenye ulemavu ambavyo nimevitaja hapo mwanzo vina wanafunzi ambao wana ulemavu wa aina mbalimbali na kuna wenye ulemavu wa viungo ambao wana changamoto kubwa ya kufanya zile kazi za kiufundi, lakini pia idadi ya walimu kwenye vyuo hivyo hailingani na idadi ya wanafunzi kwa sababu wanafunzi wale wanatakiwa sasa idadi yao iwe mwanafunzi mmoja kwa mwalimu mmoja au wanafunzi wawili kwa mwalimu mmoja.

Je, Serikali haioni haja sasa yakuvifanya hivi vyuo viwe *inclusive* ili wanafunzi wale waweze kusaidiana wenyewe kwa wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa kwenye shule ya msingi Wailesi iliyopo katika Wilaya ya Temeke kuna kitengo cha watoto wenye ulemavu wa ubongo ambao wao wanasoma pale kwenye elimu jumuishi na wanapofikia hatua fulani wanapelekwa kwenye kujifunza mafunzo ya ufundi na chuo hicho hakina mapato yoyote wala hakipewi ruzuku yoyote kutoka Serikalini.

Je, Mheshimiwa Waziri muhusika yupo tayari kufuatana na mimi kwenda kwenye hiyo Shule ya Msingi Wailesi iliyopo katika Wilaya ya Temeke? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM K.n.y. WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Mariam kwa kufuatilia watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inawajali sana watu wenye ulemavu na ndiyo maana imejenga shule ambazo mchanganyiko na watu ambao wasio walemavu ili waweze kuwasaidia katika kazi wanazozifanya na kuwapa vifaa vya kuwasaidia ili waweze kuwa na uelewa rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, Serikali ipo tayari na Wizara husika kwenda kwenye chuo hicho kuangalia mazingira yaliyopo ili kuweza kuwasaidia kwa umakini, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Iringa una idadi kubwa sana ya watu wenye ulemavu katika wilaya zake zote, lakini wamekuwa wakimaliza shule hawajui utaratibu wa kujiunga kwenye vyuo. Je, ni utaratibu gani unatumika ili waweze kwenda kujiunga kwenye vyuo vya ufundi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM K.n.y. WAZIRi MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua suala la watu wenye ulemavu na Serikali inawajali kama nilivyosema mwanzo watu wenye ulemavu kwa kuzingatia katika kupata elimu kuna vifaa mbalimbali ambavyo vinawasaidia na kufika shule kuna mazingira ambayo yanawasaidia kuwahakikisha wanapata elimu hiyo na walemavu wote wanatakiwa wajiandikishe kama sensa iliyopita ilivyoeleza, inawatambua walemavu wapo wangapi na kujua kwamba shule za walemavu tuchukue watu wangapi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunahamia Ofisi ya TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge wa Nanyamba.

Na. 531

**Ujenzi Wodi ya Wazazi Kituo cha Afya Mkwedu – Newala**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA K.n.y. MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga wodi ya wazazi katika Kituo cha Afya cha Mkwedu – Newala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dugange, Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Mkwedu ni miongoni mwa vituo vya afya 202 kongwe ambavyo vinahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa. Kituo hiki kina upungufu wa miundombinu muhimu ikiwemo wodi ya wazazi, jengo la upasuaji, jengo la maabara na jengo la kufulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itavifanyia ukarabati vituo hivyo kwa awamu kikiwemo Kituo cha Afya Mkwedu katika Halmashauri ya Newala, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kama inavyoonesha kwenye jibu la Serikali hapo kituo hiki hakuna wodi hata moja, je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kujenga angalau wodi moja ya akina mama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kituo hiki kina changamoto ya wataalamu wa mionzi kama ilivyo Hospitali ya Mji wa Nanyamba ina *X-ray* lakini hakuna mtaalamu wa mionzi. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka wataalamu katika wilaya hizi mbili za pembezoni? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kituo hiki cha Afya cha Mkwedu kina upungufu wa miundombinu muhimu ambayo inatakiwa kuwepo ili kukidhi vigezo vya kuwa kituo cha afya zikiwemo wodi za wazazi, lakini na majengo ya upasuaji na majengo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tumechukua hoja hii tutakwenda kuiweka kwenye mipango yetu kuhakikisha kwamba tunatafuta fedha haraka iwezekanavyo ili kwenda kujenga jengo la wazazi, lakini pia jengo la upasuaji ili wananchi wa Kata ya Mkwedu wapate huduma zile ambazo zinafanana na kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuhusiana na upungufu wa watumishi wa *X-ray* na *Ultrasound,* ni kweli tuna changamoto ya watumishi hawa katika soko wapo wachache sana na kila kibali cha ajira kinapojitokeza kipaumbele ambacho Serikali inatoa ni kuanza kuajiri kwanza wataalamu ambao kwenye soko wapo wachache wakiwemo hao wa *Ultrasound* pamoja na wa *X-ray*. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba kwenye kibali ambacho Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekitoa hivi karibu tutahakikisha wale ambao wanasifa wanakwenda kwenye Halmashauri hii ya Newala ili kupunguza upungufu wa watumishi wa *X-ray* na *Ultrasound*, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga wodi za watoto wachanga katika vituo vya afya vya mkoa wangu wa Singida ili kunusuru vifo vya kina mama na watoto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ramani za ujenzi wa vituo vya afya za sasa zinazingatia sana uwepo wa wodi au vyumba kwa ajili ya watoto wachanga. Kwa hiyo vituo vyote vya afya ambavyo vimejengwa zaidi ya 878 mpaka sasa vina wodi na vyumba maalumu kwa ajili ya watoto wachanga. Vituo vya afya ambavyo vilijengwa siku za nyuma vina upungufu ya miundombinu hiyo na tayari vimewekwa kwenye mpango ule wa ukarabati na upanuzi wa vituo vile kongwe tutahakikisha sehemu ya miundombinu ni pamoja na vyumba hivyo vya watoto wachanga, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kilolo kuna Vituo vya Afya vya Nyalumbu, Ilula, Ng'uluwe na Ruaha Mbuyuni havina vifaa tiba, nini mkakati wa Serikali kupeleka vifaa tiba katika vituo hivyo vya afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka miwili ya fedha 2022/2023 – 2023/2024 Serikali hii ya Awamu ya Sita imeshapeleka fedha kwenye halmashauri zote 184 zaidi ya shilingi bilioni 93 kwa ajili ya

vifaa tiba na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo imepata fedha mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya vifaa tiba na mwaka huu wa fedha zaidi ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya vifaa tiba.

Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumuelekeza na kumsisitiza Mkurugenzi na Mganga Mkuu wa Halmashauri kuweka kipaumbele kwenye vituo vya afya ambavyo vinaupungufu mkubwa zaidi wa vifaa tiba ili fedha ile inunue vifaa hivyo viende kutoa huduma katika vituo ambavyo vina upungufu mkubwa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Iwondo ili wananchi wa Kata ya Iwondo waanze kupata huduma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vituo vya afya ambavyo vimejengwa kwa awamu ya kwanza ambavyo vilipelekewa shilingi milioni 500 au shilingi milioni 400 na miundombinu muhimu ya majengo matano imekamilika, lakini vituo hivyo vyote tutaviingiza kwenye ujenzi wa awamu ya pili ambao utahusisha ujenzi wa wodi, lakini pia wodi ya wanaume, wanawake pamoja na wodi ya watoto.

Kwa hiyo naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Malima kwamba tukifika awamu ya pili tutaipa kipaumbele pia kituo hicho cha afya ili tuweze kujenga miundombinu ambayo inapungua, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Kituo cha Afya Ngome, Kituo cha Afya Ipogolo na Kituo cha Afya Isakalilo ni vile vituo ambavyo vimejengwa zamani, havina wodi za kisasa kwa ajili ya kujifungulia. Je, Serikali mnaweza mkatusaidia tupate wodi hizo kwa sababu pia tunahitaji huduma hiyo kwa haraka?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechukua hoja ya vituo vya afya vya Manispaa ya Iringa na Jimbo la Iringa Mjini na kwa bahati nzuri tumeshafanya ziara nafikiri Isakalilo pale tuliona, tulishatoa maelekezo na nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatafuta fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Jangalo, Mpendo na Lahoda ni kata za mpakani, mwaka 2003 Serikali ilifanya tathimini kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, nataka kujua ni lini sasa Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi huo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kata zote za kimkakati tayari tumeshazianisha kwa awamu, tulishaanza na awamu ya kwanza mwaka wa fedha 2021/2022, tupo awamu ya pili mwaka wa fedha 2023/2024. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatafuta fedha na kwenda kujenga vituo vya afya hivyo kwa awamu kadiri ambavyo tumeweka mpango mkakati katika nchi nzima, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunahamia swali linalofuata, swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, litaulizwa kwa niaba na...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Getere.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin Nyamoga.

Na. 532

**Kuangalia Upya Mipaka ya Tarafa ya Makambako**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA K.n.y. MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaangalia upya mipaka ya Tarafa ya Makambako ambapo kata 12 zipo Jimbo la Makambako na kata tano zipo Jimbo la Lupembe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa maeneo ya utawala katika Tawala za Mikoa ambayo hujumuisha mikoa, wilaya na tarafa hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Utaratibu wa Kuanzisha Mikoa na Wilaya, Sura 397 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kata tano za Igongolo, Ikuna, Kichiwa, Mtwango na Ninga katika Tarafa ya Makambako ziko katika Jimbo la Lupembe hali ambayo hupelekea changamoto za kiutawala baina ya Jimbo la Makambako na Lupembe. Aidha, kwa kuzingatia utaratibu wa uanzishaji au mabadiliko ya mipaka ya kiutawala kusudio hujadiliwa katika Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC)* ambayo inapokea maoni kutoka ngazi za msingi za utawala. Kamati ya

Ushauri ya Mkoa *(RCC)* itakapokea maoni ya Kamati ya Ushauri ya Wilaya na kuyajadili kisha kuyawasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inashauri halmashauri kufuata utaratibu ulioainishwa kwenye Sheria ya Uanzishwaji wa Maeneo ya Kiutawala kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Mji wa Makambako unakuwa na idadi ya watu inaongezeka na kutokana na hivyo maeneo yamekuwa madogo kwa hiyo upimaji wa viwanja na maeneo kwa ajili ya makazi na shughuli nyingine yanakosenaka.

Je, ni lini Serikali itafanya mpango wa kuongeza lile eneo ili wananchi wa Makambako waendelee kupata makazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna maeneo mengi sana kwenye nchi hii ambayo ugawaji wake haukuzingatia jiografia na kwa hiyo huwa ni shida sana kwenye utoaji wa huduma, kwa mfano mtu wa kutoka Tarafa ya Mazombe na Mahenge Ilula, maeneo ya Ilula kwenda Kilolo kupata huduma inabidi apite Iringa Mjini. *(Makofi)*

Je, Serikali ina mpango gani wakupitia maeneo haya na kuona jinsi nzuri ya kuyafanya yawe katika uwiano wa kijeografia ili kurahisisha huduma za wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna baadhi ya halmashauri au majimbo ambayo yana changamaoto ya kimipaka, lakini kwa Jimbo la Makambako Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga amefuatilia mara kadhaa kuongeza mipaka ya Jimbo la Makambako, Halmashauri ya Mji wa Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niitumie nafasi hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, lakini pia Mheshimiwa *DC* kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kufuata utaratibu wa kupata maoni kwa wananchi wa maeneo hayo ili waweze kupeleka kwenye vikao vyao vya *DCC* na vikao vya *RCC* na kukubaliana kama wilaya, lakini kama mkoa na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kuchukua hatua na hili linakwenda sambamba na ile hoja ya baadhi ya mipaka kutozingatia hali za kijiografia za maeneo hayo na kuleta changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapokea maoni kutoka kwa wadau na wadau hao ni wananchi wa maeneo hayo kwa maana ya *DCC* pamoja na *RCC* kwa ajili ya kuchukua hatua hizo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, tunashukuru, Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali fupi la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo Makambako, inafanana sana na changamoto ambayo tunayo kule Arumeru Mashariki, hususani mpaka wa Jimbo letu la majimbo mawili ya upande wa Mashariki kwa maana ya Siha na Hai. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu changamoto hiyo ya mpaka? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee kwamba ni Serikali inashauri mamlaka husika kwa maana ya *DCC* na *RCC* kukaa na kutoa mapendekezo, lakini mipaka ya Majimbo inatolewa pia na ya Tume Huru ya Uchaguzi pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, naomba wafuate taratibu hizo kuleta maoni yao ambayo

yamefuta sheria na kanuni za mwongozo ulivyo ili tuweze kuona namna gani mamlaka husika zitachukua hatua kurekebisha changamoto hizo ikiwa inawezekana kufanya hivyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa kama vile ikituchanga hivi. Unasema tupeleke mipaka ya Halmashauri Bunda na Halmashauri ya tunapokaa Jimbo la Bunda lipo tofauti. Tukapeleka vikao vyote kwenye kikao cha *DCC* na tukapeleka *RCC* na tumeleta mapendekezo yetu hapa, lakini majibu yanayotoka ni kwamba Serikali sasa hivi haina mpango wa kuendeleza mipaka ya utawala, huku tunaambiwa tupeleke.

Sasa nini jibu la Serikali kuhusu mipaka hii ili tusiwe tunapiga kelele humu ndani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwanza ilishatoa maelezo na msimamo kwamba kipaumbele kwa sasa ni kuboresha maeneo ya utawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi. Hii ni kwa sababu tuna kata, tuna halmashauri, tuna Ofisi za Wakuu wa Wilaya, kuna Ofisi za Wakuu wa Mikoa na makazi yao bado hayakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge, mara kwa mara wanaitoa hapa ni kwamba maeneo hayo yanahitaji kujengewa miundombinu ili maeneo hayo ya utawala watoe huduma bora zaidi.

Kwa hiyo, Serikali iliona ni vyema kuweka kipaumbele cha kukamilisha miundombinu hiyo kwenye mamlaka ambazo tayari zinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea haijasimama, kwa maana ya taratibu nyingine za kuomba kubadili mipaka, kuomba mamlaka mpya zinaendelea na *document* hizo zinatunzwa, muda ukifika tutazipitia *document* hizo na kufanya maamuzi kulingana na vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mhakikishie Mheshimiwa Getere kwamba yote ni sawa kwamba, tuendelee na kule maombi hayo kwa kufuata taratibu na Serikali itaendelea kuyatekeleza kulingana na vipaumbele, lakini pia muda ukifika hatua nyingine zitachukuliwa katika maeneo hayo mengine, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Wilaya ya Kishapu ina kata 29, lakini ina idadi ya watu 355,000 na ukubwa wa eneo ni kilometa za mraba 45,333; eneo hili ni kubwa sana na kimsingi Serikali ni lazima irahisishe kupeleka huduma kwa wananchi kwa kupunguza eneo la kitawala na hasa kijimbo.

Je, Serikali inasema nini kupunguza eneo hili na kuwa na majimbo mawili walau kuwarahisishia wananchi huduma za kimaendeleo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Butondo kwamba Serikali inatambua kwamba, Halmashauri ya Kishapu na Jimbo la Kishapu, ni miongoni wa majimbo makubwa na ameshawasilisha hoja hiyo mara kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee kumhakikishia tu kwamba, Serikali itachukua hatua hizo baada ya kupata taarifa rasmi kupitia vikao vya *DCC* na *RCC* na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na pale ambapo utaona sasa kuna sababu ya kufanya hivyo na muda muafaka basi hatua hizo zitachukuliwa. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba Serikali inatambua na tutachukua hatua hizo kadri itakavyowezekana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, kwa niaba, karibu Mheshimiwa.

Na. 533

**Hitaji la Uzio – Shule ya Sekondari Igunga**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA K.n.y. MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa uzio katika Shule ya Sekondari ya Igunga?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kainja. Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023/2024 Serikali imepeleka shilingi milioni 58 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili na matundu matano ya vyoo katika Shule ya Sekondari Igunga kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Mwaka 2024/2025 Halmashauri ya Igunga kupitia mapato ya ndani imetenga shilingi milioni 55 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa uzio katika Shule ya Sekondari Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa uzio kwa ajili ya ulinzi wa mali na wanafunzi wa bweni, hata hivyo,

kwa sasa kipaumbele cha Serikali Kuu ni ujenzi wa miundombinu ya msingi inayowezesha kuongeza nafasi za udahili wa wanafunzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kutokana na majibu mazuri ya Serikali, kwa kuwa Shule ya Sekondari ya Igunga, ipo mjini na bajeti ya uzio huo ni shilingi milioni 276. Halmashauri imetenga shilingi milioni 55.

Je, Serikali sasa haioni kuna haja kutoa fedha Serikali Kuu na ku-*support* uzio huu ili uweze kukamilika kwa ajili ya usalama wa watoto hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, ni lini Serikali sasa itaweza kutenga fedha kwa pamoja za majengo ya madarasa pamoja na uzio ili viende sambamba? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kupongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kweli amekuwa akifuatilia kwa ukaribu sana masuala ya elimu na hasa kwa watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza, sisi sote ni mashahidi kwamba kutokana na utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila malipo kumekuwa na ongezeko kubwa la udahili wa wanafunzi wa shule za msingi, lakini sekondari. Kwa hiyo, kwa kipindi hiki katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata udahili kuingia katika shule za msingi na sekondari, Serikali imeweka kipaumbele cha kuhakikisha inajenga miundombinu ya msingi kwa maana ya madarasa, lakini kwa maana ya maabara za sayansi, lakini kwa maana ya mabweni. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa ujenzi wa uzio katika shule zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele kwa sasa ni kuhakikisha kuna kuwa na miundombinu ya kutosha ya madarasa ili wanafunzi wote waweze kupata udahili kuingia katika shule zetu hizi za msingi, lakini shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, la Mheshimiwa Mbunge ambalo anataka Serikali Kuu iweze kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio, lakini kwa misingi ile ile ya ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zina jukumu la msingi la kutafuta bajeti, kupata mapato, lakini kuhakikisha inajenga miundombinu ya msingi ikiwepo miundombinu katika sekta ya elimu kwa maana ya madarasa mabweni na uzio.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii, kwanza kumpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Igunga kwa kutenga fedha hii shilingi milioni 55 kwa ajili ya kuanza kujenga uzio huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kutoa wito kwa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa, kuendelea kutenga fedha katika mipango na bajeti zao kwa ajili ya kujenga miundombinu muhimu kama hii ya uzio kutegemeana na hali ya eneo husika.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, Serikali tayari imeanza kujenga uzio kupitia fedha zilizotengwa katika mapato ya ndani na Mkurugenzi huyu na Serikali itahakikisha inaendelea kutenga fedha kwa utaratibu huo ili uzio uweze kujengwa kwa maslahi mapana ya wanafunzi wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, shule hizi za sekondari za kata zinakabiliwa sana na changamoto kubwa ya upungufu ya watumishi, walinzi na walezi na kwa kuwa tatizo hili sasa shule zimekuwa na wanafunzi wengi.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati sasa wa kwenda kufanya tathmini upya ili kuweka mazingira mazuri ya ulinzi wa wanafunzi wetu hawa hasa wakati wa usiku? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba arudie swali lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge naomba rejea swali lako.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa hatua inazochukua na majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hatuwezi kuweka uzio kwenye shule zote nchini kwa wakati mmoja shule za *A level* na shule nyingine zinakabiliwa na na upungufu mkubwa wa watumishi wakiwepo wale walinzi na walezi katika shule zetu. Kwa kuwa gharama ya uwekaji wa huu uzio ni mkubwa Serikali haitakiwi kufanya tathmni ya kina ili kuja na mpango mkakati wa ulinzi thabiti kwa wanafunzi wetu katika shule zetu hizi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kama nimeelewa swali lako, Mheshimiwa Mbunge unataka kujua kama Serikali inaweza kulipia gharama za walinzi kwenye shule zetu za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze kwanza, Mheshimiwa Mbunge, kwa kuendelea kufuatilia na kufuatilia hasa masuala ya ulinzi wa wanafunzi wetu na maeneo ya shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa maana ya halmashauri zetu hizi kupitia mapato ya ndani zina nafasi ya kutenga bajeti kwa ajili ya

kuhakikisha zinasimamia masuala ya msingi ikiwemo haya unayoyazungumza Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuhakikishie kwa sababu yote ni Serikali, tutaendelea na sisi kufanya tathmini na kutengeneza msukumo na kutengeneza mwongozo mzuri kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kwenye shule zetu kuna kuwa na ulinzi na wanafunzi wanaweza kusoma katika mazingira yenye amani na utulivu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari Amandus Chinguile ipo Nachingwea Mjini na imezungukwa na makazi ya watu, je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga uzio katika shule hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zina wajibu wa msingi wa kutafuta fedha, wa kutafuta mapato na kutenga kwenye bajeti zake fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya muhimu ikiwemo ujenzi wa uzio katika shule zetu. Kwa hiyo, niendelee kumkumbusha Mkurugenzi aweze kuweka katika mipango ya kibajeti katika halmashauri yake ili aweze kutenga fedha kwa kadiri ya vipaumbele na kwa kadiri ya mahitaji kwa ajili ya ujenzi wa *fence* katika shule hii ya Amandus Chinguile. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Missenyi, Serikali imejenga hosteli katika shule za sekondari na shule hizo zimejengwa pembezoni mwa makazi ya watu ili kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya vijana wetu kusoma.

Je, ni lini sasa Serikali itatujengea uzio katika Shule za Sekondari za Ruzinga, Bwabuki, Bunazi na Minziro ili wanafunzi wawe katika hali ya usalama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA**): Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza kwanza jukumu lake la msingi la kutenga bajeti kwa ajili utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya msingi katika sekta elimu. Kwa hiyo, niendelee kumkumbusha Mkurugenzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi aweze kutathmini, lakini aweze kutengeneza mipango na kutenga bajeti kwa kadiri ya vipaumbele kwa ajili ya kuendeleza miundombinu muhimu hii katika sekta ya elimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari ya Endasak, Nangwa, Mulbadaw, Balangdalalu ni za kidato cha tano na sita na zote hazina uzio.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka msukumo kwenye ujenzi wa uzio kwa sababu ya usalama wa watoto wanaosoma kwenye shule hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa miundombinu mbalimbali katika sekta ya elimu ikiwemo umuhimu wa ujenzi wa uzio. Niendelee kumhakikishia Serikali inatambua umuhimu mkubwa na itaendelea kutenga fedha kupita Mamlaka za Serikali za Mitaa, lakini kupitia miradi ya Serikali Kuu kwa ajili ya kuhakiksiha inaboresha miundombinu katika shule zetu hizi za kidato cha tano na cha sita kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali linalofuata la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 534

**Kujenga Mifereji Kudhibiti Mafuriko Tabora Mjini**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, upi mkakakati wa Serikali kujenga mifereji kudhibiti mafuriko Tabora Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa mifereji mikubwa ya maji ya mvua katika Kata za Malolo, Mpera na Mwinyi ambazo zimekuwa zikikumbwa na mafuriko wakati wa kipindi cha mvua na kubaini kuwa shilingi bilioni 18.47 zinahitajika kujenga mitaro mikubwa yenye urefu wa kilometa 25 katika Mji wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023 kiasi cha shilingi milioni 399.12 kutoka fedha za majimbo na tozo ya mafuta zilitumika kujenga sehemu ya mitaro hiyo yenye urefu wa kilometa 2.4. Pia katika mwaka 2023/2024 kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji ya Tanzania *(TACTIC)* itajengwa mifereji

mipya kwenye Barabara ya Kisarika yenye urefu wa kilometa 2.99 ambapo barabara hii inaunganisha Kata ya Mwinyi na Malolo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, maswali ya nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali shilingi milioni 399 ambazo anasema zimekwenda mwaka 2022/2023 kujenga mifereji kwa ajili ya kupunguza mafuriko hazijaonekana kufanya kazi hiyo kikamilifu kwa sababu wananchi wetu wameendelea kupata mafuriko mwaka hadi mwaka pindi mvua zinaponyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza kuniambia ni mifereji ipi ambayo imetumia fedha hizo kujengwa mitaro hiyo ili tuweze kujua ni mitaro gani ambayo imejengwa kwa ajili ya kusaidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri unaonaje tukimaliza Bunge hili mwezi Julai tuongozane ili tuweze kwenda kuona hali halisi jinsi ilivyo katika Manispaa ya Tabora? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**A NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kupambania wananchi kuhakikisha kwamba wanapata miundombinu bora ya mifereji hii ili kuzuia mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza ambalo ametaka kujua shilingi milioni 399.12 katika mwaka wa fedha 2022/2023 ilienda kujenga mifereji katika eneo gani? Kumjibu hilo fedha hii ilienda kujenga kilometa 2.2 katika Barabara ya Kombomasai - Kata ya Malolo, Navimajo - Kata ya Mpera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kwamba nipo tayari baaada ya Bunge hili la Bajeti kwenda kutembelea na kukagua eneo hilo na ujenzi wa miundombinu hii. Nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge mimi sitasubiri mpaka mwezi Julai, mwisho wa Bunge, Jumamosi hii ninatarajia kuwa Tabora na nikuhakikishie nitaenda kukagua eneo hili kujionea hali halisi na kuona kwamba fedha hii imeenda kuwanufaisha wananchi na tutaenda pamoja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selemani Kakoso, tafadhali.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi zilizojengwa na *TARURA* kwenye Wilaya ya Tanganyika zimeharibika baada ya mvua nyingi kuvunja madaraja na mifereji ikiwemo Barabara ya Ikaka - Mnyagala, Ikaka - Kamsanga. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba kutokana na mvua nyingi zinazonyesha miundombinu ya barabara maeneo tofauti tofauti imekuwa ikipata changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni kuhakikisha kwamba inaenda kufanya ujenzi wa dharura kwenye maeneo ambayo mawasiliano yamekatika ili kuhakikisha mawasiliano yanarudi, yanaunganika na yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, amenitajia barabara zake hizi, mara baada ya kutoka katika kipindi hiki cha maswali na majibu nitakaa nay echini ili aweze kuniainishia haya maeneo husika na tutayachukua sisi kama Serikali ili kuona hatua gani za dharura zinaweza kuchukuliwa ili kuhakikisha tunaunganisha mawasiliano katika maeneo aliyoyataja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia Theonest swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Kata ya Nkwenda, Kijiji cha Nkwenda ambako kunafanyika soko linalowaleta pamoja wafanyabiashara wa Kyerwa na Karagwe kuna mtaro mkubwa sana umeelekezewa kwenye hilo soko la Nkwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua mkakati wa kujengea huo mtaro ili uweze kuwa salama kwa wafanyabiashara kuepusha mafuriko ambayo yamekuwa yakitokea mara nyingi na kufanya soko au biashara ishindikane kufanyika kwenye eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa miundombinu ya barabara, mifereji na hasa katika kuchochea uchumi kwa maana ya kuwezesha shughuli za uchumi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itahakikisha inatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kuhakikisha inajenga mitaro katika eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge ili kuboresha mazingira na kuwawezesha wananchi wetu waweze kufanya shughuli zao za uzalishaji mali kwa utulivu na kwa urahisi zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mvua za *El-Nino* zimenyesha kwa kiwango kikubwa katika Halmashauri ya Itigi, Barabara ya Itigi – Damweru haipitiki kabisa, ilikuwa imejaa maji na sasa maji yameanza kukauka, lakini Barabara ya Kalangali kwenda Tulieni imeharibika kabisa haipitiki.

Je, Serikali iko tayari kutuongezea pesa za kutosha kurudisha miundombinu hii ili watu wafanye maisha yao ya kawaida?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara zetu hizi na hasa za wilaya na kama nilivyotangulia kusema kipaumbele cha Serikali katika kipindi hiki ni kuhakikisha inaunganisha mawasiliano ya barabara kwenye maeneo ambayo mawasiliano yamekatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itatafuta fedha na itatumia taratibu za dharura kuhakikisha inaunganisha mawasiliano kwenye maeneo ambayo yameathirika sana na mvua na mawasiliano yamekatika katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa uendelevu Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu hii ili iweze kuwa miundombinu imara ambayo inapitika kwa misimu yote na mwaka mzima.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunahamia Wizara ya Nishati, Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 535

**Kukatika Katika kwa Umeme katika Mji wa Biharamulo**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme katika Mji wa Biharamulo kwa kukamilisha *sub-station* ya Nyakanazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri, Wizara ya Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Nyakanazi mwezi Desemba, 2023. Aidha, kukamilika kwa kituo hicho kumeenda sambamba na ufungaji wa *circuit breakers* kwenye laini ndefu iliyokuwa inapeleka umeme katika Wilaya za Bukombe, Mbogwe, Biharamulo na Chato hii imepelekea kutenganisha matumizi ya umeme kwenye wilaya hizo na kwa sasa kila wilaya inajitegemea hivyo kupunguza kukatika kwa umeme ndani ya Wilaya ya Biharamulo. *TANESCO* inaendelea na matengenezo ya kuimarisha miundombinu ya kusafirishia na kusambaza umeme wilayani humo ili kuwe na umeme wa uhakika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nipongeze kwa hatua hizo kubwa ambazo zimefanyika za uwekezaji huo mkubwa wa Kituo cha Nyakanazi na hatimaye kuweza kutuondolea tatizo la kukatika katika kwa umeme, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa Nyakanazi tulikuwa tunapata mradi wa umeme unaotoka Biharamulo kwenda Mkoa wa Kigoma au tunauita Kigoma – Nyakanazi ambao ulikuwa na vijiji 32, vijiji saba vikiwa Wilaya ya Biharamulo katika Kata za Kalenge na Nyanza na vijiji 25 Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua sasa katika Wilaya ya Biharamulo, hivyo vijiji saba vya Kata za Kalenge na Nyanza mpaka sasa baada ya kumalizika mradi ule ni wateja wangapi wameunganishiwa umeme kutokana na vijiji hivi saba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, mradi huu mkubwa wa kutoka Geita kuja Nyakanazi na kutoka Rusumo kuja Nyakanazi ulipitia maeneo ya watu na walistahili fidia. Nadhani mwaka jana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati akiwa Biharamulo tuliomba wale watu ambao hawajalipwa pesa zao waweze kupatiwa pesa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kusikia kauli ya Serikali, mmefikia wapi na maandalizi ya kuwalipa pesa wale waliokuwa wamepitiwa na ule mradi ili sasa kwa sababu umeme unawaka na walipisha maeneo yao wao waweze kupata haki yao ya kulipwa fidia ambayo imechukua muda mrefu sana, wale waliokuwa wamebaki wachache kama 32? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, *Engineer* Ezra Chiwelesa kwa kazi nzuri anayoifanya kuwatetea wananchi wa Biharamulo na ninaomba kujibu maswali yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vijiji saba vilivyopo katika Kata za Kalenge pamoja na Nyanza mpaka sasa tumeshaunganisha wateja 615 na kwa sababu kazi hii ni endelevu, tunaendelea hivyo kadiri wananchi wanavyofanya *wiring* tunaendelea kuwaunganisha na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kazi hii inafanyika vizuri sana na *REA* kwa kushirikiana na *TANESCO*.

Kuhusu swali la pili la fidia, ipo katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza ni Geita – Nyakanazi. Kwa Geita – Nyakanazi malipo ya Serikali yaani *statutory compensation* tayari imeshafanyika kwa wananchi wote, ambacho kimebaki ni *top up compensation* ambapo mkandarasi anatakiwa kuongeza ili waweze kulipwa kwa viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshaambiwa mshauri elekezi anatarajiwa kuja hivi karibuni ili kuweza kufanya *survey* pamoja na masuala mengine ya kiutendaji ili wananchi hawa waweze kumaliziwa ile *top up compensation* ya mfadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipande cha Rusumo – Nyakanazi kulikuwa na wananchi 1,024 na wananchi takribani 986 wameshalipwa fedha shilingi bilioni 3.7 na wannchi waliobaki ni 38 tu ambapo wanadai shilingi milioni 81.02. Wananchi hawa hawajalipwa kwa sababu ya changamoto za mirathi na migogoro mingine, lakini fedha zao zipo na kadri ambavyo wataweza kukamilisha taarifa zao na kuweza kumaliza migogoro na kukamilisha taratibu za mirathi watappatiwa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, fedha za wananchi hawa zipo, taratibu zikikamilika hawa 38 waliobaki katika kipande cha Rusumo – Nyakanazi na wenyewe watalipwa fedha zao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kahama ina mkandarasi mmoja tu wa kupeleka umeme wa *REA* vijijini pamoja na halmashauri zake tatu. Sasa ilhali amezidiwa na malalamiko ni makubwa sana kwa wananchi wetu, ni nini mkakati wa Serikali wa kupeleka kila halmashauri mkandarasi wake ili kuondoa malalamiko haya kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpa pole Mheshimiwa Cherehani kwa changamoto hii ya mkandarasi. Nataka nimhakikishie kuwa tunafahamu changamoto ya mkandarasi huyu wa Kahama na tayari tumeshachukua hatua ikiwemo kukaa naye na kuweza kujua ni namna gani tunamwongezea nguvu ili aweze kuongeza kasi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Mbunge, ndani ya hizi wiki mbili, tatu mimi na yeye tuongozane twende Kahama ili tuweze kuangalia utekelezaji wa miradi hii katika eneo hili kwa sababu ni kweli kuna changamoto, lakini sisi dhamira yetu ni kutatua changamoto hizi ili wananchi wapate umeme kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunafahamu changamoto za mkandarasi na tutaendelea kumsimamia kwa weledi mkubwa sana kuhakikisha anamaliza kazi ambayo alitakiwa kuimaliza kwa wakati, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla kwa kazi ya kusambaza umeme vijijini. Mara ya mwisho nilikuwa nimekuomba kuhusiana na unyeti wa kupeleka umeme katika Vitongoji vya Songea Pori pamoja Nindi ambavyo viko mpakani na Msumbiji. Nilikuwa napenda kukumbusha na kujua labda pengine kama kuna hatua ambazo tayari zimeshaanza kuchukuliwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nianze kwa kumpongeza mama yangu Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo lake la Nyasa. Serikali kwa mwaka huu wa fedha unaokuja 2024/2025 tayari tumetenga fedha ya kupeleka umeme kaika vitongoji 4,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwamba hivi vitongoji viwili ambavyo amevitaja hapa kwa unyeti wa maeneo haya kwa sababu yako mpakani, tutazingatia ili na yenyewe yaingie katika mpango wa mwaka wa fedha unaokuja ili wananchi wa vitongoji hivyo waweze kupata umeme, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi waliopisha mradi wa umeme wa Gridi ya Taifa katika Jimbo la Tunduru Kaskazini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia kaka yangu Mheshimiwa Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kwa kazi kubwa anayoifanya katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande hiki ni muhimu sana kwetu sisi kwa sababu ni sehemu ya mradi wa kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa katika mikoa ya Mtwara na Lindi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, fidia katika eneo hili ni kipaumbele kwenye Serikali ya Awamu ya Sita na tunaendelea kufanyia kazi ili hivi karibuni wananchi hawa waanze kulipwa fidia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kaka yangu Mheshimiwa Zidadu na wananchi wa Tunduru kuwa fidia hii Serikali tunaenda kuilipa, watulie na watupe muda kidogo tumalizie taratibu ili tuanze kuwalipa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya Serikali.

Tunahamia Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Ally Yahaya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kwa niaba yake swali lake linaulizwa na Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, karibu.

Na. 536

**Ujenzi wa Bandari Kavu Nang'oba – Nanyumbu**

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga bandari kavu Nang'omba Wilayani Nanyumbu ili kuhudumia mizigo ya nchi ya Msumbiji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suala la ujenzi wa Bandari Kavu limepewa kipaumbele katika Mpango Kabambe wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* uliohuishwa wa mwaka (2021 – 2045) ambao umeweka vigezo vya ujenzi wa bandari zote kavu kwa vipaumbele kutokana na matarajio ya ukuaji wa shehena katika maeneo yanayopakana na nchi za jirani. Aidha, utafiti ulifanyika katika Bandari Kavu ya Nang'omba katika Wilaya ya Nanyumbu na kubaini kuwa bandari hiyo haijakidhi vigezo vya ujenzi wa bandari kavu vilivyotajwa hapo awali na hivyo kutobainishwa katika mpango wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa muktadha huo, Serikali inachukua wazo la Mheshimiwa Mbunge ili kulifanyia kazi kwa siku zijazo baada ya kufanya utafiti wa ukuaji wa shehena ambao ni moja kati ya vigezo vya kujenga bandari kavu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa ujenzi wa bandari kavu ilikuwa ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Tatu Hayati Mheshimiwa Mkapa, na kwa kuwa Serikali imesema haijakidhi vigezo, je, Serikali iko tayari kwenda kuwaelezea wananchi ili sasa wazo hilo lifutwe kwenye Mawazo yao kwa sababu walikuwa wanasubiria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, lengo hasa ilikuwa kuongeza uchumi kupitia shughuli za usafirishaji wa mizigo hasa kutoka Bandari ya Mtwara na kupitia Daraja la Mtambaswala lile la Umoja, je, Serikali inafikiria shughuli gani sasa ili kuweka shughuli mbadala katika lengo la awali?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mhata na Mheshimiwa Hokororo kwa maana ya swali lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapojenga bandari kavu vipo vitu unavyovitazama na kikubwa tunaangalia shehena na ndio maana kwa sasa hivi ninapozungumza, Serikali ya Awamu ya Sita inajenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma, inaunganisha mpaka Burundi, lakini pia inajenga reli kuelekea Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ushoroba huu kilometa 2,300 tunajenga Bandari Kavu ya Kurasini, Bandari Kavu ya hapa Ihumwa - Dodoma, Bandari Kavu ya Fela kule Mwanza na Katosho, Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua ya pili tukishatoka kwenye upande huu wa *central corridor* kwa maana ya *CSGR* Serikali inaendelea na mchakato kwa ajili ya kujenga reli ya kusini inayotoka kwenye bandari yetu ya Mtwara pamoja na Kisiwa Mgao, inaunganisha kwenda Liganga na Mchuchuma ambako kuna madini pamoja na makaa ya mawe, lakini inakwenda mpaka *Mbamba Bay* ambayo tayari ninavyozungumza mjenzi wa Bandari ya *Bamba Bay* yupo *site*. Sasa hii Bandari Kavu ya Nang'omba itakuwa ni bandari muhimu tukishafika hatua hiyo ili tutoe mzigo bandari tuupeleke Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutauingiza katika mchakato huu wa *southern corridor* kuhakikisha kwamba na yenyewe inakuwa sehemu ya mradi wetu wa reli hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunakushukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunahamia Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini sasa aulize swali lake. Kwa niaba.

Na. 537

**Kilimo cha Mpunga Bonde la Ibanda – Geita**

**MHE. MINZA S. MJIKA K.n.y. MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza uzalishaji wa mpunga Bonde la Ibanda na kiasi gani kinahitajika kuweka skimu ya umwagiliaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ina mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mpunga katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Bonde la Ibanda kwa kujenga bwawa na miundombinu ya umwagiliaji. Usanifu wa Bonde la Ibanda umekamilika na taratibu za manunuzi za kupata mkandarasi zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inatekeleza ujenzi wa skimu ya umwagiliaji Ibanda kupitia mkandarasi *M/S Jiangxi Geo-Engineering* kwa mkataba wenye thamani ya shilingi bilioni 13.6 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na mkataba wenye thamani ya shilingi bilioni 21.2 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa mradi huu unahusisha Wilaya mbili, Wilaya ya Sengerema na Wilaya ya Geita, wananchi wa Wilaya ya Geita walishalipwa pesa zao kupisha mradi huu. Je, lini wananchi wa Sengerema watalipwa pesa hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, lengo la mradi huu ni kuongeza thamani ya zao la mpunga. Je, kuna mradi gani mwingine ambao unaweza ukajengwa katika eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba kuna madai ya baadhi ya wananchi hususani katika Halmashauri ya Sengerema na sisi kama Serikali tunalifanyia kazi na tutaleta majibu kwa sababu lipo katika mchakato na mimi nitakuwa sehemu ya watu ambao watakwenda kuwaeleza wananchi juu ya faida za huo mradi na wale ambao watapisha na fidia ambayo watalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo hilo ni mradi gani utajengwa? Mradi ni huu huu mmoja isipokuwa tutakwenda kuwaelimisha juu ya aina ya mazao wanayoweza kuyafanya zaidi ya mpunga peke yake, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu za umwagiliaji maji katika Wilaya ya Bahi miundombinu yake ni chakavu. Nini mkakati wa Serikali wa kurekebisha skimu hizi ili wakulima waweze kupata tija?

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba maelekezo tuliyopewa Wizara ya Kilimo na Mheshimiwa Rais ni kurekebisha skimu zote chakavu nchini na kujenga skimu mpya katika mabonde yote yanayohitaji skimu mpya. Kwa hiyo, lipo katika mpango na Bahi ni mashahidi kwamba kuna fedha tumeshapeleka za awamu ya kwanza na tutaleta kwa ajili ya kurekebisha skimu zote ambazo zimebakia.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Munira swali la nyongeza.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitatu sasa Wizara ya Kilimo imekuwa ikitekeleza miradi ya umwagiliaji, lakini miradi hii inaonekana ikisuasua. Je, ni sababu gani miradi hii ya umwagiliaji imekuwa ikisuasua? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekuwa tukitekeleza miradi mingi na maeneo mbalimbali nchini na kwa sababu ukishakuwa na miradi mingi maana yake mahitaji makubwa ya fedha yanakuwa yanahitajika na wakati mwingine tumekuwa tukichelewa kutoa zile *advance payment* ndiyo maana unakuta miradi imechelewa na sisi hilo tunakiri kama Wizara, lakini sasa hivi Wizara ya Kilimo tumekaa na Wizara ya Fedha tumekubaliana kuhakikisha fedha zitakuwa zinatoka kwa wakati na wale ambao hawajalipwa watalipwa kwa wakati ili kuhakikisha miradi hii inaisha kwa kadiri ambavyo tumekubaliana kwenye yale makubaliano au mkataba.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi, *Scheme* ya Mangisa imejengwa muda mrefu na imejaa udongo na tuliomba fedha kwa ajili ya kuondoa ule udongo. Je, ni lini Serikali italeta fedha ili *scheme* ile ikaweze kuwafaidisha na kuwasaidia wakulima wa Mangisa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba jambo hili na mimi nalifahamu na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inalifanyia kazi. Sehemu ambayo ipo sasa hivi ni kwamba wanatafuta fedha ili kuhakikisha kwamba tunatoa ili iweze kuwasaidia wananchi ule mradi uweze kufanya kazi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu ya swali la Mheshimiwa Flatei Massay. Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kitulo ndiyo wanaongoza kwa uzalishaji wa viazi katika Mkoa wa Njombe na sisi kama halmashauri tumejipanga kwamba tunatakiwa tuwawezeshe kuwa na *scheme* na tulipeleka maombi kwenye Wizara yenu ya Kilimo, kujenga *scheme* katika Kata ya Kitulo ili uzalishaji wa viazi uongezeke kwa ukubwa na kwa upana wake.

Mheshimiwa Waziri, ni ipi *commitment* ya Serikali kuwasaidia wananchi wa Kitulo wawe na *scheme* ya umwagiliaji ili wazalishe viazi msimu wote wa mwaka kwa ajili ya manufaa ya uchumi wao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namthibitishia tu Mheshimiwa Mbunge, na akawaambie wananchi wa Makate, Kata ya Kitulo kwamba tutajenga hiyo *scheme* kwa sababu ni sehemu ya miradi mikubwa ambayo ipo katika kipaumbele chetu kama Wizara, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya umwagiliaji kwenye Kata za Masela na Bukangilija, Kata ya

Badi upembuzi yakinifu pamoja na usanifu umekamilika. Je, ni lini Serikali itajenga miradi hiyo ya umwagiliaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Miradi ya Masela na Bukangilija iliyoko Maswa ni kwamba tumeshamaliza upembuzi yakinifu na *feasibility study,* sasa hivi tuko katika hatua ya kumtafuta mkandarasi ili tuweze kumkabidhi *site* aanze kazi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tuna changamoto ya usikivu kidogo, tutaomba wale ambao mna-*consult* basi m-*consult* kwa sauti ya chini kwa kadiri inavyowezekana.

Waheshimiwa Wabunge, mnao-*consult,* mu-*consult* kwa sauti ya chini. Mheshimiwa Msambatavangu tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, tunao-*consult*, tu-*consult* kwa sauti ya chini kidogo ili tuweze kuruhusu usikivu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ni lini *Scheme* ya Kimbande, Mjini *Mbamba Bay* itawekewa miundombinu ili vijana wengi na hasa wahitimu waweze kunufaika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba *Scheme* ya Kimbande iliyopo Nyasa ni kwamba ipo katika mipango ya Serikali na tuko katika hatua za mwisho kuhakikisha kwamba tunatafuta mkandarasi ili ianze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je Serikali ina mkakati gani wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula katika Bonde la Mto Matandu kupitia *scheme* za umwagiliaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Bonde la Matandu lililoko katika Halmashauri ya Kilwa ni moja ya bonde ambalo sisi Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji tunalifanyia *feasibility study* ili liweze kufanya kazi kipindi chote kwa kuwa na miundombinu bora na ya kisasa. Kwa hiyo, hilo ndiyo jukumu kubwa ambalo sasa hivi tunalifanya. Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tukishamaliza tutakuja na tutazungumza na wananchi na wataona faida ya huo mradi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante, tunakushukuru kwa majibu ya Serikali kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wahesnimiwa Wabunge, kabla hatujahamia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, tuna changamoto ya nafasi za kukaa wageni, kwa hiyo, tutawatangaza wageni wa kundi B pekee sasa ili kuruhusu wawapishe wageni wengine ambao tunao nje ya Bunge.

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza, tunaye Frank Petro Mathayo kutoka Hospitali ya Benjamini Mkapa. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Angel Yaee, Mwimbaji wa Nyimbo za Injili kutoka Arusha. *(Makofi)*

Tunao wadau wa mazingira 13 kutoka Shirika la *Youth Integration and Environmental Organization. (Makofi)*

Tunao wanafunzi 61 na walimu 14 kutoka Shule ya Awali ya Msingi ya Daystar ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 90 na walimu watano wa Shule ya Awali ya Msingi ya Joyful kutoka Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, miongoni mwa wanafunzi hawa kuna mtoto anaitwa Janis ambaye ni mjukuu wa Mheshimiwa Balozi Mulamula. Janis karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 100 na walimu kumi wa Shule ya Msingi ya Angelico Lipan ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine watatambulishwa baadaye. Tuliwatambulisha hawa ili kutoa nafasi kwa ajili ya wageni wengine wa Wabunge.

Tunawashukuruni sana wageni wetu kwa kututembelea Bungeni. Kama Bunge tunafarijika sana tunapoona mnatutembelea na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali. Sasa ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namwita Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 538

**Mkakati wa Kukomesha Ajali za Barabarani**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kukomesha kabisa ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu wengi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Aah, samahani kidogo, mnisamehe, mazoea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge Wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka mikakati madhubuti itakayosaidia kukomesha ajali za barabarani ambayo ni kuifanyia marekebisho Sheria ya Usalama Barabarani ambapo muswada wa sheria umeshawasilishwa Bungeni na kusomwa kwa mara ya kwanza.

Pili, kuboresha miundombinu ya barabara na kuweka alama za matumizi ya barabara; tatu, kuandaa utaratibu wa kufunga mifumo ya TEHAMA barabarani ili kufuatilia na kudhibiti ajali; na nne, kuandaa utaratibu wa ukaguzi wa lazima wa vyombo vya moto ili kudhibiti ubora wa vyombo hivyo viwapo barabarani na kuendelea kutoa elimu ya usalama barabarani kupitia vituo vya luninga na redio, elimu kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo, vituo vya mabasi, vituo vya bodaboda na bajaji, vituo vya ukaguzi wa magari, shule za udereva na kutoa mafunzo kwa madereva wa Serikali, taasisi za umma na watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kuna marekebisho kidogo, swali hili limejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Sagini na amelijibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Felista Njau, tafadhali.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, nimeona wameainisha wanatoa mafunzo kupitia luninga na redio, lakini ajali nyingi zina-*base* kwenye bodaboda na hawa hawana muda kabisa wa kusikiliza redio wala kuangalia luninga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini mkakati madhubuti wa Serikali kuhakikisha bodaboda wanapata elimu ya usalama barabarani ili kuepuka athari hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kumekuwa na ucheleweshwaji wa ulipwaji wa bima ya ajali kwa watembea kwa miguu na bodaboda, lakini inaonekana kuna kucheleweshwa kwa nyaraka kutoka Polisi. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha nyaraka hizi zinapelekwa kwa wakati ili kunusuru afya za wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Serikali, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ipo tabia hii ambayo vijana wa bodaboda wanajifunza uendeshaji wa pikipiki bila kulazimika kuingia vyuoni na ndiyo maana kwa kutambua changamoto hiyo imeelekezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Makamanda wa Polisi wa Mikoa, Maafisa wa Usalama Barabarani wa Wilaya *(DTOs* na *RTOs)* wameandaa mikakati maalumu ya kuwatembelea kwenye vituo vyao na kuwapa mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafarijika baadhi ya maeneo Waheshimiwa Wabunge wameshiriki kutoa motisha kwa hawa Maafisa wa Usalama Barabarani kuwafundisha vijana hawa ikiwa ni pamoja na kuwakatia leseni za udereva wa vyombo hivi vya moto. Kwa hiyo, nina imani hali hiyo ikiendelea walio wengi watafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili, juu ya bima za ajali na nyaraka kuchelewa Polisi ni maelekezo yetu ya Serikali kwa Makamanda wote wa Mikoa kuwasimamia *RTOs* na *DTOs* wasiwe vikwazo vya kuchelewesha nyaraka ambazo ni msingi wa waliopata ajali hizi kulipwa bima kwa mujibu wa sheria, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINA S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ajali nyingine za bodaboda zinatokana pengine na kutokuwa na maeneo rasmi ya maegesho hususani katika maeneo mengine ya viwanja vya ndege wanapokuwa wanagombea abiria.

Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa kutenga maeneo maalumu ya maegesho kwa bodaboda na bajaji jirani na maegesho ya magari ili wasigombanie abiria na kusababisha ajali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mbunge Mabula ni ya msingi na kwa sababu maeneo menhi haya yako kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa iliwahi kuelekezwa na wao ni Wajumbe wa Kamati za Usalama Barabarani ngazi za Wilaya na Mikoa na hata makao makuu, wafikirie kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya vijana wanaoendesha pikipiki maarufu kama bodaboda ku-*park*, kufanya maegesho na hivyo kuwa na utaratibu mahususi wa kuwachukua abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, vijana hawa katika maeneo mengine wameshapiga hatua ya ustaarabu kwa sababu wana vikundi vinavyotambulika, wana mfumo wa uongozi na vilevile hujipangia huyu wa kwanza, akimaliza anafuata wa pili, hiyo inaondoa uwezekano wa kunyang’anyana abiria, ambapo inakuwa sehemu ya chanzo cha ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa makundi yote ya bodaboda katika mikoa na wilaya zote kutumia utaratibu kama huo ili kwanza kuboresha mfumo wa usafirishaji na la pili ni kuepuka ajali za barabarani, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya kupata *flow* nzuri ya mjadala wa maswali na kwa sababu anayejibu ni Mheshimiwa Naibu Waziri huyo huyo, tutaruka maswali ya Wizara ya Afya, tutahamia kwanza Wizara ya Katiba na Sheria.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Josephat Simkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Hitaji la Mahakama ya Wilaya – Matai Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya katika Mji Mdogo wa Matai, Wilayani Kalambo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kalambo ni miongoni mwa wilaya zenye changamoto ya miundombinu chakavu ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa huduma za Mahakama ya Wilaya zinapatikana katika Jengo la Mahakama ya Mwanzo Matai. Aidha, zabuni ya ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kalambo ambayo pia itajumuisha Mahakama ya Mwanzo ya Matai imeshatangazwa na ujenzi unatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika kwa taratibu za manunuzi, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ya kututia matumaini, naomba niulize maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa ahadi juu ya ujenzi wa Mahakama katika Tarafa ya Kasanga, Mji Mdogo wa Kasanga, naomba kujua je, ujenzi huu utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna uchakavu mkubwa sana katika Mahakama za Mwanzo katika Wilaya ya Kalambo. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba unafanyika ukarabati katika Mahakama za Mwanzo ikiwepo Mahakama ya Mwimbi, Mwaje na zingine zote ili *at least* ziendane na hadhi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umuhimu wa kujenga Mahakama ya Mwanzo katika Tarafa ya Kasanga, tunapokea ombi hili, lakini nimweleze Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote kwamba sekta ya Mahakama kwa muda mrefu kwa kweli ilichelewa kuanza mkakati wake wa kuboresha sekta nzima ya Mahakama hususani kwenye miundombinu na hata ajira za Mahakimu na Majaji, lakini kwa miaka ya hivi karibuni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati anasisitiza juu ya utoaji wa haki kwa wananchi ameamua kuimarisha Mahakama hizi kwa kuanza mkakati maalumu wa kuzijenga Mahakama hizi. Hivi sasa tunajenga Mahakama Kuu ngazi ya mikoa nane, lakini ngazi ya wilaya zaidi ya Mahakama 20 zinajengwa na kwenye ngazi ya Mahakama ya Mahakama za Mwanzo tunajenga zaidi ya Mahakama 62. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimweleze Mheshimiwa Mbunge pale hali ya fedha itakapo ruhusu Mahakama ya Kasanga aliyoirejea hapa pia itafikiwa na kukarabatiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkakati wa kukarabati Mahakama zilizochoka, vilevile ni sehemu ya kuimarisha huduma

za utoaji wa haki. Tunavyoendelea kujenga Mahakama mpya kule ambako haziko, lakini zile zilizochakaa sana pia zinakarabatiwa. Kwa hiyo, Mahakama zako za Mwanzo ulizozirejea pia zitakarabatiwa, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Suma Ikenda, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, je, ni lini Serikali itakarabati Mahakama za Mwanzo zilizoko Masoko, Katumba, Lupata na Ikama Wilayani Rungwe ukizingatia hizo Mahakama zina hali mbaya sana? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali ya kibajeti, kwa mwaka huu katika Mkoa wa Mbeya tutakarabati na kujenga upya Mahakama za Mwanzo za Lupa Tingatinga, Ndobo, Madibira na Mbalizi. Hizi za maeneo ya Rungwe zitafikiwa pia kwa kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya Serikali.

Tunahamia Wizara ya Afya, Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 539

**Elimu ya Lishe Nchini**

**MHE. TAMINA HAJI ABASS** aliuliza: -

Je, mwenendo wa utoaji wa elimu ya lishe nchini ukoje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tamima Haji Abbas, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa utoaji wa elimu ya lishe nchini unaonesha maendeleo mazuri na umeendelea kuimarika kutokana na juhudi mbalimbali za Serikali pamoja na wadau na mwitikio mkubwa wa wananchi. Serikali imepanua wigo wa uelimishaji na uhamasishaji wa masuala ya lishe kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo: -

(i) Matumizi ya vyombo vya habari kama vile redio, televisheni na mitandao ya kijamii kote nchini na katika mikusanyiko ya kijamii;

(ii) Uwepo wa mtaala wa elimu ambao umejumuisha masuala ya afya na lishe kwa ngazi ya msingi na sekondari unaotoa fursa kwa wanafunzi kupata uelewa wa elimu ya lishe;

(iii) Wizara imezindua Mwongozo wa Kitaifa wa Chakula na Ulaji wenye lengo la kuhamasisha matumizi sahihi ya chakula mchanganyiko kwa kuzingatia vyakula vinavyopatikana hapa nchini;

(iv) Elimu ya lishe imeendelea kutolewa katika vituo vya kutoa huduma za afya kote nchini hususani wakati wa Kliniki za mama na mtoto; na

(v) Uhamasishaji kupitia Ujumbe wa Mbio za Mwenge mwaka 2024 ambao una kauli isemayo; "Lishe sio kujaza tumbo, zingatia unachokula." *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tamina Haji Abass.

**MHE. TAMINA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, wataalamu wa elimu ya lishe wanaotoa elimu ndani ya maeneo yetu wanakidhi mahitaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa kuna mikoa 12 yenye lishe duni nchini, je, Serikali ina mikakati gani ya ziada ambayo itapeleka elimu zaidi ili kuondokana nahali hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Tamina Haji Abass kwa maswali yake mawili mazuri kwamba je, wataalamu wanaotoa elimu ya lishe wanakidhi mahitaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukiri bado hatuna wataalamu wa kutosha wa masuala ya lishe, lakini kwa sababu tume-*integrate*, tumejumuisha masuala ya lishe katika mitaala ya wanafunzi wetu, kwa hiyo, walimu wetu ambao wanasomea ualimu pia, kwa hiyo wanapata mada katika masuala ya lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu katika bajeti yetu tunaanza kutoa *diploma* ya masuala ya lishe maana zamani ilikuwa ni *degree,* lakini sasa hivi tunaanza kutoa *diploma* ya lishe, tunaamini tutapata Maafisa Lishe wengi ambao wataweza kufanya kazi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu pia kwamba mikoa 12 yenye lishe duni mnafanya nini, tuna mambo makubwa mawili, la kwanza kupitia utekelezaji wa Siku ya Afya na Lishe ya Kijiji (SALIKE) ambapo tumeelekeza kila kijiji, kila mtaa katika kila baada ya miezi mitatu kukutana, kuhamasishana na kuelemishana masuala ya lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaamini kupitia utekelezaji wa Siku ya Afya na Lishe ya Kijiji tutaweza pia kusambaza elimu ya lishe kwa makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tumezindua mpango wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii ambao tutakuwa na vijana wawili, mmoja wa kike mmoja wa kiume katika kila kitongoji cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katika kila mtaa kwa maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hawa pia ndiyo watakuwa askari wa mwanzo *(front liners)* katika kuelimisha masuala ya lishe na masuala mengine ya afya kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nianze kwa kumpongeza sana Profesa Janabi kwa kuendelea kutoa mafunzo ya lishe bila kuchoka. *(Makofi)*

Je, Serikali ipo tayari sasa kushusha mafunza hayo ya lishe kwenye kata kwa wanawake hususani wanawake wa Kilimanjaro ambapo utayarishaji ndiyo muhimu kuliko hata kuwa na hivyo vitu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mama Shally Raymond kwa kweli amekuwa ni balozi mzuri wa kuhamasisha masuala ya lishe kwa wanawake wa Kilimanjaro na ninaamini wanawake wa Kilimanjaro wataendelea kumuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Profesa Janabi kwa kweli tunamshukuru na lakini pia tumepokea maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kupitia Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Musukuma kwamba elimu pia iwe *customized,* iwe inalenga makundi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kumtumia Profesa Janabi, lakini pia tutawatumia au tunaendelea kutumia wataalamu wengine wa lishe kutoka Taasisi yetu ya Chakula na Lishe, lakini pia wataalamu wa lishe ambao wapo katika halmashauri mbalimbali ili kuelimisha masuala ya lishe.

Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mnapokaa katika bajeti za halmashauri zetu tuhoji ni mikakati gani au ni *intervention* gani zinatekelezwa katika masuala ya lishe zaidi ya semina za wataalamu wa afya. Tunataka kuona wataalamu wakienda katika vijiji, katika mitaa, katika kliniki kutoa lishe na siyo ile bajeti ya lishe shilingi 1,000 ikatumika kwa ajili ya safari na semina za watumishi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri unajua mikoa inayoongoza kwa ualishaji ndiyo mikoa inayoongoza kwa udumavu, ni upi mkakati wa Wizara kwa sababu halmashauri mpaka sasa zimeshindwa wa kuweza kutoa elimu ili kuleta matokeo chanya?

**MWENYEKITI:** Ahsante, kwa ufupi.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Aida Khenani kwa kweli amezungumza ukweli mikoa ambayo ndiyo wazalishaji wakuu wa chakula ikiwemo Njombe, Rukwa, Katavi, Iringa na Kagera ndiyo pia wana kiwango kikubwa cha utapiamlo hususani kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati kama nilivyoisema changamoto siyo upatikanaji wa chakula, changamoto ni wananchi kuandaa chakula lakini pia na kula chakula mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Novemba, 2023 kwa mara ya kwanza tumezindua Mwongozo wa Kitaifa wa Chakula na Ulaji, mwongozo huu unahimiza katika vyakula tunavyokula kuzingatia makundi sita ya vyakula. Kundi la kwanza ni nafaka, lakini pia kundi la pili ni masuala ya vyakula vya asili ya wanyama, kundi la tatu vyakula vya asili ya kunde na mbegu za mafuta, kundi la nne ni mboga mboga, kundi la tano ni matunda, kundi la sita ni mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aida Khenani niseme tumepata fedha kutoka kwa wadau, tumeamua kidogo tusimame tuangalie zinakwenda kufanya kazi gani kwa sababu siyo tu fedha nyingi zinapelekwa, lakini tunataka kuona interventions ambazo zitagusa wananchi. Kwa upande wa Njombe tumeona wanawake pia hawana muda wa kulisha watoto kwa sababu ni wachapakazi wakubwa sana. Kwa hiyo ndiyo maana pia tunataka kuanzisha vituo vya malezi ya awali ya watoto ambapo pia masuala ya lishe yataweza kufanyiwa kazi na kuhimizwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rehema Juma Migilla tafadhali.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Mheshimiwa Waziri Serikali huwa inatenga shilingi 1,000 kwa ajili ya masuala ya lishe kwa watoto wetu chini ya miaka mitano, lakini mimi kama mwakilishi wa wananchi sijawahi kuona matumizi ya zile fedha hata siku moja kwenye halmashauri zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali kuhusu matumizi ya fedha hizo kwa walengwa wetu ambao ni watoto wa chini ya miaka mitano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rehema Migilla amesema jambo zuri na nimelisema, kwanza tunaona ongezeko la shilingi 1,000 zinazotengwa kwa ajili ya lishe

katika halmashauri mbalimbali, kwa hiyo na mimi naomba nirudishe jukumu kwenu Waheshimiwa Wabunge kuangalia pia au kufuatilia matumizi ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya kutekeleza hafua za lishe katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia fursa hii kuwataka Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, lakini na Wakurugenzi wetu wa Halmashauri kuhakikisha fedha zile shilingi 1,000 zinazotengwa kwa ajili ya kutatua changamoto za lishe zitumike kwenye masuala yenye tija yanayogusa moja kwa moja wananchi na siyo mambo ambayo hayana tija.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anastazia Wambura.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, wataalamu ambao wamehitimu *degree* ya lishe katika nchi yetu ni wengi na wapo mitaani. Je, Mheshimiwa Waziri atakubali sasa kwamba wawaajiri wale ambao wamemaliza waliohitimu *degree* ya lishe? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Anastazia Wambura kwa swali lake zuri kuhusu wataalamu. Kama nilivyosema ni kweli tunao wataalamu katika ngazi ya *degree* ambapo tumejitahidi katika halmashauri nyingi sasa hivi angalau tuna Afisa Lishe, lakini tumeona ili tufanye vizuri zaidi tunahitaji Maafisa Lishe katika ngazi ya chini na tunaamini tukiwapata pia wa ngazi ya *diploma* wataweza pia kufika rahisi zaidi kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kukuhaidi katika nafasi za ajira tutaongeza ajira kwa maafisa lishe lakini nitawaomba sana basi wasitake kubaki mjini wawe tayari kufanya kazi katika halmashauri zote ikiwemo halmashauri za pembezoni ambazo ndizo zina changamoto kubwa ya lishe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ahsante kwa majibu ya Serikali kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir sasa aulize swali lake.

Na. 541

**Ushirikiano kati ya *TBS* na *ZBS***

**MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR** aliuliza: -

Je, kwa kiasi gani ushirikiano kati ya *TBS* na *ZBS* unaleta matokeo chanya na kusaidia kutatua changamoto za wajasiriamali hususani kutoka Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* limekuwa na mashirikiano na Taasisi ya Viwango ya Zanzibar kwa maana ya *(ZBS)* kupitia Hati ya Makubaliano *(Memorandum of Understanding - MoU*) ya zaidi ya miaka tisa sasa. Ushirikiano huu kati ya *TBS* na *ZBS* unaendelea kuleta matokeo chanya kwa kutatua changamoto za wajasiriamali wakiwemo kutoka Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kutekeleza mifumo ya uandishi wa viwango, usimamizi wa ubora, upimaji na ugezi na hivyo kusaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora na zenye viwango vya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ameir.

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri kwa ruhusa yako ningeomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa moja kati ya majuku ya msingi sana ya *TBS* na *ZBS* ni kulinda usalama wa chakula kwa mlaji. Swali langu ni kwamba je, tathimini ikoje sasa juu ya huu uwepo wa vifaa

vyenye teknolojia ya kisasa vyenye uwezo wa kuchambua sampuli kwa uharaka sana wa vyakula vyetu ili kumuhakikishia Mtanzania kwamba anakula chakula chenye usalama na uhakika?

(b) Swali langu la pili ni kwamba je, kuna jitihada gani zozote au viashiria vyovyote vya mafanikio mpaka sasa kwa wafanyabiashara ambao wana-*standard mark* ya *ZBS* kuweza kupata soko la biashara zao kikanda na Kimataifa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kwanza na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Ameir kwa kufuatilia sana kuhusiana na mashirikiano na ubora wa bidhaa kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie wewe, lakini na Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania imekuwa kati ya nchi ambazo zina maabara ya kisasa sana ya kupima ubora na viwango kwa ajili ya usalama katika chakula na bidhaa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako tu wakati Kamati yako ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma ilipotembelea *TBS* ilijionea dhahiri maabara ya kisasa katika jengo ambalo tumejenga kwa zaidi ya shilingi bilioni 20 na maabara ya kisasa ya zaidi ya shilingi bilioni 500 ambazo hizi zinatumika kupima ubora kwa ajili ya kuhakikisha bidhaa na hasa chakula zinakuwa na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna teknolojia za kisasa na vifaa vya kisasa kabisa ambavyo vina hithibati ya Kimataifa vinavyopima ubora kwa ajili ya usalama wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili kuhusiana na bidhaa zenye ubora ambazo kutokana na ushirikiano wa *ZBS* na

*TBS* ambazo zinazaliwa kutoka kule Zanzibar, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwanza kwamba sisi kama nchi ni Wajumbe wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afika *(SADC)* ambapo kule kuna tuzo za Kimataifa kwa maana ya Kanda hiyo *SADCAS* na katika tuzo hizo za ubora tumekuwa tukishirikisha *ZBS* na *TBS* na wajasiriamali na wazalishaji wengi kutoka Zanzibar wamekuwa vinara wa kuonesha bidhaa bora zinazokidhi matakwa na soko la Kimataifa lakini la kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika tuzo hizo moja ya kampuni ambazo zimepata tuzo ni Kampuni ya Zanzibar *Milling Cooperation* kupitia unga wake maarufu sana wanasema *special boflo* ambao umekuwa ukipata tuzo karibu miaka yote kwenye mashindano hayo. Hata wajasiriamali wadogo wa kawaida kwa mfano *Zanzibar Zaidat Product* amekuwa pia naye anapata tuzo nyingi za uzalishaji kwa bidhaa zake katika tuzo hizo ambazo zinashirikisha mataifa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *ZBS* na *TBS* wanashirikiana kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara, lakini na Zanzibar zinakuwa na ubora kwa ajili ya kupata soko la Kimataifa, lakini na ndani ya nchi, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa niaba ya Serikali.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Hoja ya Dharura.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba mniruhusu nitangaze kwanza wageni tulionao Bungeni na tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge ukiachana na wale ambao nimeshawatangaza.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambaye ni mdogo wake kutoka Bukoba, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa David Kihenzile ambaye Naibu Waziri wa Uchukuzi ambao ni wapiga kura wake kutoka Mufindi Kusini, Mkoa wa Iringa, karibuni sana wapiga kura. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Agnes Hokororo ambaye ni mdogo wake kutoka Mkoa wa Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Stansalaus Mabula ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Suma Fyandomo ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Agnes Marwa ambao ni Madiwani kutoka Wilaya ya Serengeti, Mkoa wa Mara, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Tunao wagei wageni watatu wa Mheshimiwa Khalifa Suleiman ambao ni viongozi wa CCM Wilaya ya Kati Kusini Unguja, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Omar Ali Omar ambao ni wanachama wa Chama cha Mazingira na Ufugaji wa Tija Tanzania (CHAMAUTA) kutoka kanda ya Pemba Kaskazini, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni wanafamilia na kipekee wameongozwa na mama mzazi wa Mheshimiwa Boniphace Butondo, mama yetu Mama Chitirika pamoja na Daktari Mbusa, karibuni sana, sana, sana kwa ajili ya familia nzima ya Mheshimiwa Boniphace Butondo tunawashukuru wanafamilia. *(Makofi)*

Tunao wageni wa watano wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kutoka Taasisi ya Medea Tanzania ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni ambao tulishakwisha watangaza lakini naona nakosa karatasi moja ya wageni, Sekretarieti, ahsante.

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 51 na walimu watano kutoka *Veritas Extended Primary School* iliyopo Kimara, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna wageni wa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ambao ni Majid Hamad na Mheshimiwa Kessy Sharif ambao ni Madiwani wa Kata Gongoni, karibuni sana Bungeni. Naamini ni wa chama chetu, tunakushukuru sana Mheshimiwa Hawa na ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ambao ni wapiga kura wake kutoka Tabora Mjini, ahsante sana na karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hilo naomba nitoe matangazo muhimu. Mheshimiwa Aida tafadhali.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 54 na kwa ajili ya kuokoa muda naomba nisiisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli ya uvuvi ni shughuli halali kwa mujibu wa Katiba yetu ya nchi na wananchi wanafanya shughuli hizo kwa ajili ya uchumi na kwa ajili ya kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ya Tanzania iliingia kwenye makubaliano na nchi nne kwa ajili ya kusimamisha shughuli za uvuvi kwa muda wa miezi mitatu ndani ya miaka mitatu. Bunge lako Tukufu tarehe 14 Mei, lilipitisha kusimamisha shughuli za uvuvi Ziwa Tanganyika na hivi ninavyozungumza hali ni

mbaya sana kwa wavuvi hawa kwa sababu wamekata leseni kwa ajili ya shughuli ya uvuvi, lakini wamekopa mikopo benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hata uwezo wa kununua maharage au mchicha hawana hiyo fedha, wakati Bunge lako Tukufu linaendelea hali ya Watanzania hawa uwezo wa kumudu milo mitatu kwa siku inashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa jambo hili na kwa kuwa ni shughuli halali siyo shughuli haramu, ninatoa hoja ili Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono tujadili kwa maslahi ya Watanzania kwa kuwa hawajavunja sheria yoyote ya Tanzania na kati ya hizo nchi nne, ni nchi mbili tu ndiyo zimetekeleza hilo agizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja Wabunge wenzangu waniunge mkono ili tuweze kujadili jambo hili kwa maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuketi kwanza, naomba tuketi tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ilitakiwa nisikilize hoja alafu atoe maelezo na baada ya kutoa maelezo ndipo mpate fursa ya kuunga mkono hoja, Mheshimiwa Aida kanuni unazifahamu.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Aida Khenani kwa Kanuni ya 54 ya Kanuni zetu za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 jambo ambalo amelieleza ni jambo ambalo linahusu utekelezaji wa mkataba na kwa *nature* ya mikataba siyo jambo la dharura, lakini pia tuna fursa ya mijadala ya Bajeti Kuu na Mheshimiwa Spika naamini atatoa muda kwa Mheshimiwa Aida Khenani kuweza kulileta hili jambo kwenye mjadala wa Bunge na Serikali itoe majibu kuhusu jambo hili au itazame namna bora ya kutekeleza mkataba huu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nina matangazo; tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo tarehe 5 Juni, 2024

kutakuwa na semina kuhusu Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa Kutumia Riba ya Benki Kuu ya Tanzania itakayotolewa na Wizara ya Fedha. Semina hii itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu.

Tuna tangazo lingine kinatoka kwa Mwenyekiti wa Umoja Wabunge Wanawake Tanzania, Mheshimiwa Shally Raymond anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanawake kuwa tarehe 7 Juni, 2024 mara baada ya kuahirishwa kikao cha Bunge saa 4.00 asubuhi kutakuwa na kongamano litakalofanyika katika ukumbi wa Mabele wote mnakaribishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho siku ya Alhamisi, tarehe 6 Juni, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 4.41 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 6 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*

## 5 JUNI, 2024